

---

## DOKEZO SABILI

---

**KWENDA KWA:** WAFANYAKAZI WOTE  
**KUTOKA KWA:** AFISA UTUMISHI NA UTAWALA  
**TAREHE:** 22/02/2018

---

### **YAH: ZOEZI LA UHAKIKI WA WATUMISHI KWA KUTUMIA TAARIFA ZA VITAMBULISHO VYA TAIFA**

Husika na mada tajwa hapo juu.

Kama mnavyofahamu Serikali ilianzisha mchakato wa kuhakiki watumishi wake kwa kutumia taarifa za vitambulisho vya Taifa zilizoingizwa katika mfumo wa 'Lawson'. Ofisi ya TAFIRI Makao Makuu kwa kushirikiana na Maafisa Utawala wa Vituoni imekuwa ikiratibu mchakato wa utekelezaji wa zoezi hilo.

Hata hivyo hadi sasa ripoti iliyochukuliwa kutoka katika mfumo wa 'Lawson' inaonesha kuwa kuna watumishi ambao bado hawajahakikiwa. Katika orodha hiyo wapo watumishi ambao hawajawahi kuwasilisha vitambulisho vyao kabisa na wengine ambao walishawahi kuwasilisha vitambulisho vyao lakini bado mfumo unaonesha hawajahakikiwa kutokana na taarifa zao za NIDA kutotumwa katika 'Lawson'.

Kwa barua hii ninawaomba watumishi wote walioorodheshwa hapo chini bila kujali wapo katika kundi gani wawasilishe tena nakala za vitambulisho vyao kwa Maafisa Utawala ili viweze kuwasilishwa Makao Makuu ambapo vitahakikiwa upya. Tarehe ya mwisho ya kupokea vitambulisho hivyo ni 02/03/2018.

Tunaomba msamaha kwa usumbufu utakaojitokeza kwa wale ambao walishawasilisha vitambulisho vyao katika awamu zilizopita.

Ninatanguliza shukurani zangu za dhati.



Jackson E. Payowela,

**Kny. AFISA UTUMISHI NA UTAWALA.**

